# HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

Ofisiya Mkurugenzi
Mtendaji (W)
S.L.P. 355,
**Handeni**
**Tanga,**

Simuyamdomo: 027 2977402
Tel Fax: 027 2977402
Email: *ded@handenidc.go.tz*

.

**TAARIFA YA MAFANIKIO YA KUSULUHISHA MIGOGORO YA ARDHI HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI**

Migogoro ya mipaka ya maeneo ni moja ya changamoto kubwa iliyokuwa inaikabili Halmashauri ya Wilaya ya Handeni na kukwamisha maendeleo kwa namna moja ma nyingine .Kwakuliona hilo Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imefanikiwa kutatua jumla ya migogoro nane(8) iliyokuwepo katika Wilaya hadi kufikia februari mwaka 2017.

Migogoro hii ambayo ilikua iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imetatuliwa kwa ushirikiano baina ya ofisi ya Mkuu wa Wilaya ikiongozwa na Mh. Godwin Gondwe Mkuu wa Wilaya ya Handeni, ofisi ya Mkurugenzi ikiongozwa na Bw. William Makufwe Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni na wataalam wa ardhi.

Mbinu zilizotumika zilikua ni pamoja na kukutanisha serikali za pande zote zenye migogoro na kufafanua mipaka kwa mujibu wa ramani za upimaji wa vijiji wa mwaka 2007 na kwa migogoro ya mipaka kati ya Wilaya na Wilaya GN(Tanagazo la Serikali) imetumika kufafanua na kuainisha mipaka yenye migogoro. Aidha, kuanzia tarehe 03/09/2016, zoezi lilifanyika kama ifuatavyo:-

**Kijiji cha Kibindu na Muungano B**

Zoezi la kukutanisha serikali za vijiji husika lilifanyika tarehe 03/09/2016 ambapo pande zote mbili zilisikilizwa ili kubaini ni eneo lipi linalohitaji ufafanuzi. Baada ya hapo, wataalam wa Ardhi walionesha na kufafanua mipaka iliyopo kwa mujibu wa ramani za mwaka 2007 na kubaini kuwa eneo lenye utata lipo katika kijiji cha Muungano B.

**Kijiji cha Gendagenda na Kwabojo**

Zoezi la kukutanisha serikali za vijiji husika lilifanyika tarehe 06/09/2016 ambapo pande zote mbili zilisikilizwa ili kubaini ni eneo lipi linalohitaji ufafanuzi. Baada kusikiliza pande zote mbili, wataalam wa Ardhi waliwaonesha wajumbe ramani ya mwaka 2007 na kufafanua mipaka iliyopo kwa mujibu wa ramani hiyo ambayo inaonyesha kwamba:-
Kijiji cha Kwabojo, kwa upande wa mashariki kinapakana na Hifadhi ya msitu wa Gendagenda, kaskazini kinapakana na kijiji cha Komsanga, na kusini magharibi kinapakana na kambi ya Mgambo JKT.

Kijiji cha Gendagenda, kwa upande wa magharibi kinapakana na Hifadhi ya msitu wa Gendagenda. Kaskazini kinapakana na kijiji cha Kwadoya. Pia, makutano ya Reli na barabara ya Mgambo kwenda Pangani ni ndani ya kijiji cha Gendagenda. Eneo la kijiji cha Kwabojo halivuki reli kama walivyokuwa wanajua, kwani eneo hilo ni la kijiji cha Gendagenda.

**Kweditilibe na Konje katika Mtaa wa Mankinda**
Tarehe 07/09/2016, Mh. Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Handeni, pamoja na wataalam wa Ardhi wa Halmashauri zote mbili, Waliwakutanisha wananchi wa mtaa wa Mankinda na Konje na kufafanua GN iliyotenga mipaka ya Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Mji. Kwa mujibu wa G.N, Mtaa wa Mankinda upo Halmashauri ya Mji katika Kata ya Konje.

**Nyasa na Madebe**
Tarehe 20/09/2016 uongozi wa pande zote mbili ulikutanishwa na kupewa nafasi ya kuelezea eneo lipi linalohitaji ufafanuzi. Wataalam wa Ardhi walionesha na kufafanua mipaka iliyopo kwa mujibu wa ramani za mwaka 2007 iliyoonyeha kuwa eneo lenye utata lipo katika kijiji cha Nyasa. Mpaka wa Nyasa na Madebe umepita katika umbali wa takribani kilomita 3.7 kutokea katika eneo hilo lilikuwa na utata kuelekea katika kijiji cha Madebe.

**Kwamatuku na Kweingoma**
Tarehe 07/10/2016 uongozi wa pande zote mbili ulikutanishwa na kufafanuliwa mipaka ya vijiji vyao kwa mujibu wa ramani za upimaji wa vijiji za mwaka 2007 ambazo zinaonyesha kuwa, eneo lililohitaji ufumbuzi lipo katika kijiji cha Kwamatuku. Pia, Ramani ya Msitu wa Hifadhi ya mwaka 2007 ilifafanuliwa na kuonyesha kuwa eneo hilo lilitengwa na Kijiji cha Kwamatuku kuwa eneo la Hifadhi ya Msitu.

**Gole (Halmashauri ya Wilaya ya Handeni) na Negero (Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi)**
Tarehe 08/10/2016 Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Handeni na Kilindi, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Handeni na Kilindi pamoja na wataalam wa Ardhi, waliwakutanisha viongozi wa vijiji vya Gole na Negero katika eneo ambalo linahitaji ufumbuzi. Wataalam wa Ardhi walifafanua mipaka ya Halmashauri (W) Handeni na Kilindi kwa mujibu wa G.N ambapo eneo husika lilionekana kuwa lipo ndani ya mipaka ya Halmashauri (W) Handeni katika Kijiji cha Gole.

**Shamba la Mkonge la Kwamgwe**
Tarehe 18/10/2016 Mh. Mkuu wa Wilaya akiambatana na Kamati ya ulinzi na Usalama ya Wilaya Handeni, Mkurugenzi Mtendaji, na Wataalam mbalimbali wa Halmashauri pamoja na wawekezaji wa shamba la mkonge AMC LTD walifanya ziara ya kuongea na wananchi namna ya kuachia maeneo ambayo wananchi hao walivamia katika shamba hilo kwa kufanya makazi na kilimo hali iliyopelekea mwekezaji huyo kushindwa kuendelea na shughuli zake.

Baada ya kuainisha mipaka ya shamba hilo la mwekezaji, wananchi waliovamia walikubali kuwa wapo ndani ya shamba hivyo waliomba kupewa eneo la kilimo katika shamba hilo ili waendelee kulima mazao ya kudumu ambapo mwekezaji alikubali kutoa ekari 500 kwa Kijiji cha Bondo. Wananchi wengine watakaokuwa wanahitaji kuendelea kulima mazao ambayo sio ya kudumu katika shamba hilo la mwekezaji, watatakiwa kuandika barua za maombi. Pia, wananchi waliarifiwa kuwa ambao wanaishi kwenye nyumba za mkonge wataendelea kuishi ila wasiendelee kujenga zingine. Vile vile nyumba za ibada, shule na zahanati ambazo tayari zimejengwa katika shamba hilo, zitaendelea kutumika bila kuharibiwa.

Uongozi wa Halmashauri uliwataka wawekezaji AMC LTD kuwasilisha Mpango kazi wa utekelezaji wa shamba hilo kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Handeni.

**Manga na Mazingara katika kitongoji cha Kwedichocho**

Viongozi wa vijiji vya Manga na Mazingara pamoja na viongozi wa kata za Mazingara na Mkata walikutanishwa mnamo tarehe 19/10/2016 ili kupata ufafanuzi wa mipaka kwa mujibu wa Ramani za upimaji wa vijiji wa mwaka 2007. Kwa mujibu wa ramani hizo kitongoji cha Kwedichocho kipo katika kijiji cha Mazingara.

Viongozi wa vijiji vyote vyenye migogoro, waliagizwa kuacha malumbano juu ya mipaka kwakuwa tayari wameshafafanuliwa mipaka hiyo na kutakiwa kuheshimu Ramani za mwaka 2007. Pia waliagizwa kufuata taratibu na sheria katika ugawaji wa Ardhi ya Kijiji kwa wananchi au wawekezaji.

Sambamba na hilo, walikumbushwa kuwa kila mwananchi anaruhusiwa kuishi au kufanya shughuli zake popote bila kuvunja sheria, hivyo basi watu wanaoishi au kufanya shughuli zao katika Kijiji jirani wanatakiwa kufuata sheria na taratibu zilizopo katika eneo husika ili kuepusha migogoro.

kufanya shughuli zao katika Kijiji jirani wanatakiwa kufuata sheria na taratibu zilizopo katika eneo husika ili kuepusha migogoro.

Aidha Mkuu wa Wilaya aliwataka wananchi kujikita katika suala zima la maendeleo kwani muda mwingi unatumiwa kusuluhisha migogoro badala ya kuhamasisha shughuli za maendeleo. Aliwaeleza kuwa yeye hana mamlaka ya kubadili ramani ya mwaka 2007 mwenye idhini ya kubadili matumizi ya ardhi ni Rais peke yake Mipaka Hivyo basi Mipaka iliyopo kwa sasa kwa mujibu wa ramani za upimaji (2007) na GN iheshimiwe ili kuepuka migogoro ya mara kwa mara..

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya Wilaya ya Handeni aliwaeleza wananchi wote kwamba lengo kuu lilikua sio kubadili alama za mipaka ya maeneo yao bali ni kuwapa uelewa wa mipaka yao na kwamba hakuna mtu anayekatazwa kufanya shughuli halali za maendeleo kwenye ardhi ya Tanzania isipokuwa kwa kufuata Sheria, Taratibu na Kanuni za mahali husika.

Alda Sadango

Afisa Habari

Halmashauri ya Wilaya Handeni